




JARIDA LA TARIME DC



Mkuu wa Mkoa alipokelewa na Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Wilaya, Kaimu Mkurugenzi na Viongozi wengine wa kitoka SENAPA na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime katika Jengo la Utawala Nyamwaga, Tarime



Tarehe 01/02/2024, Mkuu wa Mkoa Mhe. Said Mtanda afika katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kwa ajili ya Uzinduzi wa Miradi ya "UJIRANI MWEMA", iliyoanzishwa na kukamilishwa na Serengeti National Park (SENAPA) wakishirikiana na Tanzania National Park (TANAPA) pamoja na Uongozi wa Halmashauri ya Tarime. Mkuu wa Mkoa asindikizwa na Mkuu wa Wilaya Col. Michael M. Mntejele, Katibu Tawala wa Wilaya, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime pamoja na Viongozi wengine kutoka SENAPA, TANAPA na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime

Mradi wa kwanza uliotembelewa na kuzinduliwa na Mhe. Said Mtanda ni Mradi wa Madarasa matatu yaliyojengwa Shule ya Msingi Kegonga kata ya Nyanungu. Mradi wa pili ni Nyumba ya Walimu (3 in 1) ambayo imejengwa Shule ya Msingi Byantang'ana, iliyopo kata ya Kwihancha. Miradi hiyo imejengwa na SENAPA ili kuimarisha mahusiano kati yao na Wananchi wa vijiji vinavyozunguka Mbuga ya Wanyama Serengeti.

Baada ya Uzinduzi wa Miradi hiyo, Mkuu wa Mkoa ametoa shukrani kwa SENAPA na TANAPA kwa kazi nzuri ya kuboresha maisha ya Wananchi hasa wanaoishi karibu na Mbuga hiyo na amesilhi wananchi kuheshimu utaratibu wa kuingia mbugani ili kuhakikisha amani kati yao na uongozi wa Mbuga ya Wanyama Serengeti



**HABARI
NJEMA**



VIONGOZI WAPOKELEWA KWA SHANGWE HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



Tarehe 01/02/2024, Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe. Said Mtanda afika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ili kuzindua Miradi ya "UJIRANI MWEMA". Miradi hiyo ni Madarasa matatu yaliyojengwa Shule ya Msingi Kigonga na Nyumba ya Walimu (3 in 1) iliyojengwa Shule ya Msingi Byantang'ana. Miradi hiyo ilianzishwa na Serengeti National Park wakishirikiana na Tanzania National Park (TANAPA) na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kwa ajili ya kuhakikisha mahusiano mazuri kati ya Uongozi wa mbuga ya Wanyama Serengeti na Wananchi wa vijiji vya karibu na mbuga hiyo

Mkuu wa Mkoa pamoja na Viongozi waliomsindikiza katika uzinduzi wa Miradi hiyo akiwemo Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Wilaya, Kaimu Mkurugenzi, na viongozi wengine kutoka SENAPA, TANAPA na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime wapokelewa kwa shangwe na Furaha na Wananchi wa kata hizo.

Baada ya uzinduzi wa Miradi hiyo, Mhe. Said Mtanda ameshukuru sana kwa mapokezi mazuri na kahakikisha kufikisha salamu zao kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pamoja na hayo ameahidi kutatua changamoto alizopokea kutoka kwa wananchi hao